OFFICE OF THE GENERAL
INTERNATIONAL HEADQUARTERS

**Ujumbe wa Jenerali wa Krismasi ya mwaka 2022**

Ninapofikiria kuhusu nyota iliyokuwa sehemu muhimu ya hadithi ya Krismasi, nakumbushwa kwamba wanasayansi huzitizama nyota angani kwa njia tofauti. Wao hutumia miaka ya mwanga kupima umbali wa nyota kutoka tulipo duniani. Mwaka wa mwanga ni umbali ambao mwanga husafiri katika mwaka mmoja wa dunia, kwa hiyo ni karibu maili trillion 5.88 (au kilometa trillion 9.46).

Jua ndiyo nyota ya karibu sana na sisi nayo iko umbali wa maili milioni 93 kutoka kwetu. Kwa hiyo, mwanga wa jua huchukua karibu dakika 8 na sekunde 20 kutufikia, ikimaanisha tunaliona jua kama lilivyokuwa dakika 8 zilizopita. Nyota inayofuata kwa ukaribu na sisi ni – Alpha Centauri – ipo karibu umbali wa miaka ya mwanga 4.3, kwa hiyo tunapoitizama nyota hii leo, tunaiona kama ilivyokuwa miaka 4.3 iliyopita. Ni kama tunaangalia nyuma ili kuendana na wakati.

Hii ina maana kwamba yaliyoandikwa katika Mathayo 2:1- 2 waliiona nyota ambayo mwanga wake ulikuwa unaangaza kabla hata hawajaiona. Na bado, Mungu aliitumia ile nyota kuwaongoza wamfikie Yesu: 'Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia' (Mathayo 2:2).

Yesu alikuja ili awe Nuru ya Ulimwengu. Alikuja kuangaza nuru yake katika giza – giza letu, giza la dunia hii. Tunasoma katika Isaya 9:2: 'Wale watu waliokwenda katika giza wameona nuru kuu; wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, nuru imewaangaza.' Haya yalitolewa unabii kabla Yesu hajazaliwa.

Je, tunazungumza kuhusu miaka ya mwanga tunapo mzungumzia Yesu? Hapana, sidhani ni hivyo, kwasababu Biblia inatwambia kwamba yeye ndiye Alpha na Omega - Mwanzo na Mwisho. Yeye bado ni Nuru inayoangaza leo kama alivyokuwa mwanzoni, au wakati alipokuja duniani awe mkaaji na 'aingie katika jamii' (Yohana 1:14 *Ujumbe*).

Yesu hafungwi na muda. Yeye ndiye 'nuru ya ulimwengu' (Yohana 8:12) na huangaza Nuru yake katika sehemu zenye giza nene za dunia yetu yenye matatizo, na kuleta mabadiliko. Nuru imekuja! Hakuna miaka ya mwanga inayoweza kututenganisha na Nuru hii. Yeye yuko hapa, anatufahamu, nasi tunaweza kutembea na kuzungumza naye sasa. Lengo la kuja kwake ni kuwa pamoja nasi, lakini amekuwepo, na siku zote atakuwepo, pamoja nasi.

Kama bado haumfahamu, wewe vile vile unaweza kuifahamu Nuru hii ya Ulimwengu. Jina lake ni Yesu, na alikuja ulimwenguni kuleta mabadiliko. Kama unatafuta mabadiliko, mtafute Yesu. Kama unaishi maeneo yenye giza maishani, mtafute yeye ambaye ni Nuru ya Ulimwengu.

Kwa wale ambao tayari wanamfahamu Yesu, anatukumbusha kwamba sisi ni nuru ya ulimwengu. Katika Mathayo 5:14 (*ujumbe*) tunasoma: 'Mko hapa kuwa nuru, kuzileta rangi za Mungu ulimwenguni. Mungu sio siri afichwe. Tunakwenda kwenye umma na tangazo hili, la wazi kama mji juu ya mlima.'

OFFICE OF THE GENERAL
INTERNATIONAL HEADQUARTERS

Hebu na uwe chanzo cha nuru katika kona yako ulimwenguni Krismasi hii, unaposambaza nuru ya Ulimwengu kwa wengine!

Mungu akubariki zaidi katika msimu huu wa Krismasi!

*Brian Peddle*
*General*